## Kusoma Zaidi

# Ukanushaji

Ni hali ya kukataa au kukana kauli fulani.Ukanushaji hutegemea nafsi mbalimbali na nyakati au hali inayorejelewa.

**Ukanushaji wa wakati uliopita LI**

Katika wakati uliopita, tunatumia **-ku-** pamoja viambishi vya nafsi husika.

| Wastani | Ukanushaji |
|---|---|
| a) John alimsaidia Jane. | John **haku**saidia Jane. |
| b) Nilikuheshimu sana. | **Siku**kuheshimu sana. |
| c) Yeye alikula. | Yeye **haku**la. |
| d) Mimi nilisoma. | Mimi **siku**soma. |
| e) Sisi tulicheza. | Sisi **hatuku**cheza |

**Kukanusha hali timilifu ME**

Kiambishi cha ukanushaji cha hali timilifu ni **-ja-**.Kiambishi hiki hutumika pamoja na viambishi vya nafsi husika.

| Wastani | Ukanushaji |
|---|---|
| a) Mwalimu amemlisha mtoto chakula. | a) Mwalimu **haja**mlisha mtoto chakula. |
| b) Watoto wamefagia darasa. | b) Watoto **hawajaf**agia darasa. |
| **c)** Mama amepika chakula kitamu**.** | **c)** Mama hajatupikia chakula kitamu. |

**Kukanusha wakati uliopo NA**

Katika nafsi ya kwanza,ya pili na ya tatu mtawalia, kiambishi cha ukanushaji katika wakati uliopo ni **si, hu, ha** katika umoja na **ha, ha, ha** katika wingi.

Kwa mfano,

| **Umoja** | | **Wingi** | |
|---|---|---|---|
| **Wastani** | **Ukanushaji** | **Wastani** | **Ukanushaji** |
| Mimi ninasoma. | Mimi **si**somi. | Sisi tunasoma. | Sisi **ha**tusomi |
| Wewe unapika. | Wewe **hu**piki. | Nyinyi mnapika. | Nyinyi **ha**mpiki. |
| Yeye anafua. | Yeye **ha**piki. | Wao wanapika. | Wao **ha**wapiki. |